ISSN 0856 - 034X

THE UNITED REPUBLIC OF TANZANIA

***Supplement No. 25*** ***1st July, 2022***

## *SPECIAL SUPPLEMENT*

*to the Special Gazette of the United Republic of Tanzania No.25. Vol.103 dated 1st July, 2022*

Printed by the Government Printer, Dodoma by Order of Government

TANGAZO LA SERIKALI NA. 478X la tarehe 1/7/2022

SHERIA YA NGUVU ZA ATOMU,
(SURA YA 188)

## KANUNI

*(Zimetengenezwa chini ya vifungu vya 69 na 70)*

# KANUNI ZA ADA NA TOZO ZA NGUVU ZA ATOMU, 2022

MPANGILIO WA KANUNI

*Kanuni* *Jina*

1. Jina.
2. Matumizi.
3. Tafsiri.
4. Ada ya leseni na usajili ya shughuli mbalimbali.
5. Ada za ukaguzi wa idhini za awali na ufuatiliaji.
6. Ada na tozo kwa shughuli zinazohusiana na madini ya mionzi.
7. Ada za uchunguzi wa mionzi kwenye bidhaa za vyakula.
8. Ada za huduma mbalimbali.
9. Kufutwa.

## MAJEDWALI

TANGAZO LA SERIKALI NA. 478X la tarehe 1/7/2022

SHERIA YA NGUVU ZA ATOMU,

(SURA YA 188)

**KANUNI**

*(Zimetengenezwa chini ya vifungu vya 69 na 70)*

KANUNI ZA ADA NA TOZO ZA NGUVU ZA ATOMU, 2022

Jina

**1**. Kanuni hizi zitajulikana kama Kanuni za Ada na Tozo za Nguvu za Atomu, 2022.

Matumizi

**2**. Kanuni hizi zitatumika kwa shughuli, utendaji wa kazi mbalimbali na huduma zinazotolewa na Tume

Tafsiri

**3**. Katika Kanuni hizi, isipokuwa kama muktadha utahitaji vinginevyo:

Sura ya 188

"Sheria" maana yake ni Sheria ya Nguvu za Atomu;

"kundi la kwanza" maana yake ni vyanzo hatari sana vya mionzi ambavyo visipodhibitiwa na kulindwa kwa usalama vinaweza kusababisha madhara makubwa kwa mtu anayeshughulika navyo au kuguswa navyo ndani ya dakika chache;

"kundi la pili" maana yake ni vyanzo hatari vya mionzi ambavyo visipodhibitiwa kwa usalama au kulindwa kwa usalama vinaweza kusababisha madhara makubwa kwa mtu anayeshughulika navyo au kuguswa navyo ndani ya muda wa saa kadhaa au siku;

"kundi la tatu" maana yake ni vyanzo hatari vya mionzi ambavyo visipodhibitiwa kwa usalama au kulindwa kwa usalama vinaweza kusababisha madhara ya

kudumu kwa mtu anayeshughulika navyo au kuguswa navyo ndani ya muda wa siku kadhaa;

"kundi la nne" maana yake ni vyanzo vya mionzi ambavyo vinauwezo mdogo wa kuleta madhara au uwezekano mdogo wa kusababisha madhara ya kudumu kwa mtu yeyote;

"kundi la tano" maana yake ni vyanzo vya mionzi ambavyo vinauwezo mdogo sana wa kuleta madhara au uwezekano mdogo sana wa kusababisha madhara ya kudumu na kama vikitawanywa havitaleta madhara ya kudumu kwa watu;

"Tume" maana yake ni Tume ya Nguvu za Atomu Tanzania iliyoanzishwa chini ya kifungu cha 5 cha Sheria;

"Waziri" maana yake ni Waziri mwenye dhamana na masuala ya nguvu za atomu;

"idhini ya awali" maana yake ni zoezi la kufanya ukaguzi kabla ya kuidhinisha matumizi mapya ya mionzi;

"utafutaji" maana yake ni michakato au shughuli ikijumuisha uchunguzi unaofanywa kwa madhumuni ya kubainisha au kugundua kama kuna madini ya mionzi kwenye eneo au mahali Fulani; na

"usafirishaji" maana yake ni mizigo inayosafirishwa kwenda nchi nyingine au kuingia ndani ya nchi kwa njia ya meli, treni, ndege, au gari lingine kwa wakati mmoja.

Ada ya leseni na usajili ya shughuli mbalimbali

**4**. Tume itatoza ada katika namna na njia zilizoainishwa katika Jedwali la Kwanza kuhusiana na kila leseni inayotolewa chini ya Sheria na kanuni zake.

Ada za ukaguzi wa idhini za awali na ufuatiliaji

**5**.-(1) Tume itatoza ada ya ukaguzi wa idhini za awali na ufuatiliaji katika namna na njia zilizoainishwa katika Jedwali la Pili kuhusiana na kila shughuli ya ukaguzi iliyobainishwa chini ya Sheria na kanuni zake.

(2) Tume itatoza ada kwa wazalishaji na wasambazaji wa mnyororo wa bidhaa za vyakula ndani ya

nchi katika namna na njia zilizoainishwa katika Jedwali la Nne.

Ada na tozo kwa shughuli zinazohusiana na madini ya mionzi

**6**. Mtu ambaye anakusudia kufanya shughuli yoyote iliyoidhinishwa inayohusiana na utafutaji, uchunguzi, uchimbaji na uchakataji wa madini ya mionzi au urani, atapaswa, kabla ya kufanya shughuli hiyo, kulipa ada kwa Tume kwa namna iliyoainishwa katika Jedwali la Tatu.

Ada za uchunguzi wa mionzi kwenye bidhaa za vyakula

**7**. Tume itatoza ada kwa uchunguzi wowote wa mionzi kwenye mnyororo wa bidhaa za vyakula na bidhaa zinazohusiana kwa namna iliyoainishwa katika Jedwali la Nne.

Ada za huduma mbalimbali

**8**. Tume inaweza, kupitia makubaliano, kutoa huduma zinazohusiana na kazi zake zilizoidhinishwa na huduma hizo zinaweza kutozwa katika namna iliyoainishwa katika Jedwali la Tano.

Kufutwa TS. Na. 366 la 2011

**9**. Kanuni za Ada na Tozo za Nguvu za Atomu, 2011 zinafutwa.

*Tangazo Na. 478X (Linaendelea)*

**JEDWALI LA KWANZA**

*(Limetengenezwa chini ya kanuni ya 4)*

ADA ZA KUTOA LESENI/USAJILI WA SHUGHULI MBALIMBALI

1. Maombi ya idhini ya Vifaa vya Kuzalisha Mionzi na Vyanzo vya Mionzi kwa huduma za hatibabu na zasizo za kimatibabu, kibali cha utafiti na vyuma chakavu.

| NA. | AINA YA HUDUMA | ADA AU TOZO (TZS) |
|---|---|---|
| 1 | Kupata idhini ya kutumia, kumiliki, kuendesha, kukodisha, kuingiza ndani ya nchi, kusafirisha nje au kuhamisha vifaa vya uchunguzi wa kimatibabu. | 200,000/= kwa kila kifaa. |
| 2 | Kupata idhini ya kutumia, kumiliki, kuendesha, kukodisha, kusafirisha nje ya nchi au kuingiza ndani nchini *CT Scanner*, vifaa tiba (*teletherapy na brachytherapy*), *angio-suite*, Picha za MRI (*Medical Resonance Imaging)*, Dawa za nyuklia, *Positron Emmission Tomography-CT* na vifaa vya mnururisho wa mionzi. | 300,000/= kwa kila kifaa. |
| 3 | Kupata idhini ya kutumia, kumiliki, kuendesha, kukodisha, kuhamisha, kutoa nje ya nchi au kuingiza ndani ya nchi vifaa vya kutoa mionzi isiyo ya kimatibabu, vituo vya mawasiliano, majengo ya kuhifadhi vyanzo vya mionzi na kibali cha utafiti | 300,000/= kwa kila kifaa, kwa kila kituo, au kwa kila tafiti. |
| 4 | Kupata idhini ya kutumia, kumiliki, kukodisha, kendesha, kutoa nje ya nchi, kuingiza ndani ya nchi au kuhamisha bidhaa ya leza ya daraja la 4; *cyclotron*, kichapuzi cha Linear kisichokuwa cha kimatibabu (*Non-Medical Linear Accelerator*), X-rei isiyobadilika au Vifaa vya Mionzi kwa Majaribio yasiyo ya uharibifu, kitambazaji cha ukaguzi wa mizigo au kontena, au vifaa vingine vya hatari kubwa, sampuli za udongo zenye vyanzo vya mionzi, mionzi ya asili (*NORMs)*; na uchunguzi wa shehena ya vyuma chakavu | 500,000/= kwa kila kifaa au kwa kila shehena |
| 5 | Kupata idhini ya kutumia, kumiliki, kukodisha, kuhamisha, kuendesha, kutoa nje ya nchi au kuingiza ndani ya nchi chanzo cha kunururisha mionzi ya viwandani au kinu cha utafiti wa nguvu za Nyuklia, madini yenye vyanzo vya | TZS 5,000,000/= kwa kila huduma, na kila kimoja |

*Tangazo Na. 478X (Linaendelea)*

| | | |
|---|---|---|
| | mionzi. | |
| 6 | Kupata idhini kwa ajili ya utambuzi wa eneo, ujenzi, uendeshaji au kutengua (*decommissioning*) Kinu cha Nyuklia cha Uzalishaji wa umeme. | 10,000,000/= kwa kila huduma |
| 7 | Ada ya nyongeza kwa ajili ya kupata idhini ya kuagiza vifaa au vifaa vyote vya kutoa mionzi ya ayonaizi na isiyo ayonaizi vyenye umri zaidi ya miaka 8 tangu kutengenezwa | 1,000,000/= kwa kila kifaa |

2. Usajili wa wataalamu, watoa huduma za kiufundi na leseni ya kusafirisha vyanzo vya mionzi.

| NA. | AINA YA HUDUMA | ADA AU TOZO ( TZS) |
|---|---|---|
| 1 | Kwa usajili wa wataalamu waliohitimu kutoa huduma ya mionzi ya ayonaizi kwa watu. | Hakuna malipo |
| 2 | Kwa usajili wa wataalamu wanaoendesha, kusimika, kukarabati na kufanya matengenezo ya vifaa au mitambo ya vifaa vinavyotoa mionzi. | 50,000/= kwa kila miaka mitano (5), |
| 3 | Kwa kibali cha kusafirisha vyanzo vya mionzi vya kundi la kwanza hadi kundi la tano, madini yenye viasili vya mionzi na mionzi ya asili (NORMs) ndani ya nchi na au vinavyopita nchini | 1,000,000/= bila kujumuisha gharama zingine. |
| 4 | Kwa kibali cha utoaji huduma za kiufundi kama vile vipimo vya mionzi kwa wafanyakazi, ufuatiliaji wa mionzi mahali pa kazi, vipimo vya mionzi kwenye mazingira, vipimo vya kimaabara, ukarabati na matengenezo ya vifaa vya kinyuklia, usambazaji wa vifaa vya mionzi; usafirishaji wa vifaa vya mionzi, uhifadhi wa vifaa vya mionzi, watoa mafunzo ya ulinzi na usalama wa mionzi, ugezi na udhibiti ubora wa vifaa vya mionzi. | 1,000,000/= kwa kila huduma bila kujumuisha gharama zingine |

## JEDWALI LA PILI

*(Limetengenezwa chini ya kanuni ya 5(1))*

ADA ZA UKAGUZI WA AWALI NA UFUATILIAJI

*Tangazo Na. 478X (Linaendelea)*

Maombi ya ukaguzi usio rasmi kwa vituo vya mionzi au shughuli za mionzi za kimatibabu na zisizo za kimatibabu utatozwa kama ifuatavyo:

| NA. | AINA YA SHUGHULI | ADA ( TZS) |
|---|---|---|
| 1 | Kwa ajili ya tathmini na ukaguzi wa idara ya radiolojia. | 100,000/= kwa kila kifaa bila kujumuisha gharama zingine. |
| 2 | Kwa ajili ya tathmini na ukaguzi wa vifaa vinavyotoa mionzi, vituo vya mawasiliano, vituo vya kuhifadhia vyanzo vya mionzi na huduma nyinginezo zenye madhara madogo na ya wastani. | 200,000/= kwa kila kifaa au kwa kila kituo bila kujumuisha gharama zingine. |
| 3 | Kwa ajili ya tathmini na ukaguzi wa bidhaa za Leza daraja la 4, *Linear Accelerator*, mashine za x-rei au vifaa vilivyosimikwa kwa matumizi ya vipimo visivyoharibika, mashine za kukagua mizigo na makontena, au CT scan, Picha za MRI, maghala ya vyuma chakavu na vifaa vingine vinavyoweza kusababisha madhara makubwa. | 500,000/= kwa kila kifaa au kwa kila ghala, bila kujumuisha gharama zingine. |
| 4 | Kwa kila tathmini au ukaguzi wakati wa utambuzi wa eneo, ujenzi, makabidhiano, uendeshaji na uondoshaji wa migodi yenye madini yanayotoa mionzi ya asili au migodi ya kawaida, tathmini ya mkusanyiko wa gesi ya radoni katika migodi ya chini ya ardhi, kituo cha kunururisha mionzi ya viwandani | 5,000,000/= kwa kila huduma au kwa kila mgodi bila kujumuisha gharama zingine. |
| 5 | Kwa kila tathmini na ukaguzi wakati wa utambuzi wa eneo, ujenzi, makabidhiano , uendeshaji na uondoshaji wa kinu cha kuzalisha umeme wa nyuklia, Kinu cha Utafiti wa Nyuklia, mgodi wa madini yenye mionzi, uchakataji, uteketezaji na sehemu za kuhifadhia taka za mionzi | 10,000,000/= kwa kila huduma bila kujumuisha gharama zingine. |

## JEDWALI LA TATU

*(Limetengenezwa chini ya kanuni ya 6)*

*Tangazo Na. 478X (Linaendelea)*

ADA NA TOZO ZA SHUGHULI ZINAZOHUSIANA NA UTAFUTAJI, UCHUNGUZI, UCHIMBAJI NA UCHAKATAJI WA MADINI YANAYOTOA MIONZI

| NA. | AINA YA SHUGHULI | ADA (TSHS) |
|---|---|---|
| 1. | Kibali cha utafutaji wa madini ya mionzi | 20,000,000/= kwa mgodi |
| 2. | Kibali cha utambuzi wa eneo na ujenzi wa mgodi au Kituo cha Uchakataji. | 15,000,0000/= kwa mgodi |
| 3. | Kibali cha uchimbaji au uchakataji wa madini yanayotoa mionzi | 20,000,000/= kwa Kila leseni ya uchimbaji |
| 4. | Kibali cha usafirishaji wa madini yanayotoa kiwango kikubwa cha mionzi na yale yanayosafirishwa nje ya nchi kupitia nchini | 7,000,000/= Kwa kila mzigo |
| 5 | Kibali cha kuondosha na kufunga mgodi au kituo cha kuchakata madini | 20,000,0000/= kwa kila mgodi/ Kituo |
| 6 | Uhakiki wa uondoshaji wa uchakataji wa madini ya mionzi na vituo vyake | 20,000,000/= kwa mwaka kwa mgodi au kituo cha uchakataji. |

## JEDWALI LA NNE

*(Limetengenezwa chini ya kanuni za 5(2) na 7)*

ADA ZA UCHUNGUZI WA MIONZI KATIKA MNYORORO WA BIDHAA ZA CHAKULA NA BIDHAA ZINAZOHUSIANA

Kundi A: Kwa Uingizaji wowote wa Mnyororo wa bidhaa za Chakula, Tumbaku na Bidhaa zinazotokana na Tumbaku ndani ya nchi zitatozwa kama ifuatavyo:

1. Bidhaa za mbolea hazitatozwa.
2. Bidhaa ambazo thamani ya shehena ambayo malipwani haizidi kiasi cha Shilingi za Kitanzania milioni moja hazitatozwa.
3. Asilimia 0.4 ya malipwani ya shehena inayoingia nchini yenye thamani ya zaidi ya Shilingi milioni moja hadi Shilingi bilioni moja za Kitanzania.
4. Shilingi za Kitanzania milioni nne kwa shehena inayoingia nchini yenye malipwani inayozidi shilingi za Kitanzania bilioni moja.

Kundi B: Kwa usafirishaji wowote nje ya nchi wa mnyororo wa bidhaa za vyakula ikiwemo mbolea, tumbaku, bidhaa za tumbaku na vyakula vya msaada vinavyoingia nchini vitatozwa kama ifuatavyo:

*Tangazo Na. 478X (Linaendelea)*

1. Shehena ambazo thamani ya malipwani haizidi kiasi cha dola za kimarekani elfu mbili au kiwango sawa kwa shilingi za kitanzania hazitatozwa.
2. Asilimia 0.1 ya malipwani ya shehena yenye thamani ya zaidi ya dola za kimarekani elfu mbili au kiwango sawa kwa shilingi za kitanzania hadi Shilingi bilioni moja za Kitanzania.
3. Shilingi za Kitanzania milioni mbili kwa shehena inayotoka nje ya nchini yenye malipwani inayozidi shilingi za Kitanzania bilioni moja.

Kundi C: Nakala ya Ziada ya Cheti cha Uchunguzi wa Mionzi

Kila nakala ya ziada iliyoidhinishwa ya Cheti cha Uchunguzi wa Mionzi iliyotolewa chini ya kundi A na B ya Jedwali hili kwa shehena hiyo hiyo itatozwa shilingi za Kitanzania elfu kumi

Kundi D: Kwa wazalishaji, wasambazaji, wasindikaji na wasagaji/wachanganyaji wa bidhaa za mnyororo wa Vyakula, Tumbaku na bidhaa za Tumbaku na wamiliki wa na watumiaji wa maji ya visima na hifadhi ya maji:

i. Ada za uchunguzi wa mionzi wa bidhaa za mnyororo wa vyakula, tumbaku na bidhaa za tumbaku kwa wazalishaji, wasambazaji, wasindikaji na wasagaji/wachanganyaji zitachajiwa kama ifuatavyo:

    1. Kampuni ndogo sana na kampuni ndogo hazitatozwa.
    2. Shilingi za Tanzania laki mbili na hamsini (250,000) kwa kampuni ya ukubwa wa kati.
    3. Shilingi za Tanzania laki tatu (300,000/=) kwa kampuni kubwa

    MUHIMU:

    Kwa mujibu wa Sera ya Maendeleo ya Kampuni Ndogo na za ukubwa wa Kati (2003), Tanzania imeainisha makundi ya makampuni kama ifuatavyo:

    a) Kampuni ndogo sana na Kampuni Ndogo zenye wafanyakazi wanne au mtaji uliowekezwa kwenye mashine hauzidi milioni 5.
    b) Kampuni ndogo zilizo rasimishwa na zina wafanyakazi kati ya 5 na 49 au zenye uwekezaji wa mtaji kati ya shilingi za Kitanzania milioni 5 na milioni 200.
    c) Kampuni za zilizo ajiri watu kati ya 50 na 99 au zenye uwekezaji wa mitaji kati ya shilingi milioni 200 na shilingi milioni 800.
    d) Kampuni kubwa zilizo ajiri wafanyakazi wasiopungua 100 au yenye uwekezaji wa mtaji wa mitambo ya zaidi ya shilingi milioni 800.

ii. Kwa leseni ya uchunguzi wa mionzi, umiliki, utumiaji wa maji ya visima na hifadhi ya maji

    Shilingi za Kitanzania 50,000/= kwa leseni ya uchunguzi wa mionzi ya kumiliki na kutumia maji chini ya ardhi na hifadhi ya maji kila baada ya miaka mitatu.

*Tangazo Na. 478X (Linaendelea)*

**JEDWALI LA TANO**

*(Limetengenezwa chini ya kanuni ya 8)*

ADA NA TOZO ZA SHUGHULI AU HUDUMA ZINGINE ZINAZOHUSIANA NA MIONZI

| NA. | AINA YA HUDUMA | TOZO |
|---|---|---|
| 1. | Kutoa huduma ya kutengeneza muundo na mpangilio wa kituo cha mashine ya uchunguzi wa x-rei, mapitio ya vifaa kinga vya mionzi, kufanya vipimo vya udhibiti wa ubora wa vifaa vya uchunguzi wa mionzi na kupima ubora wa vifungashio vya vyanzo vya mionzi kwa usafiri na matengenezo ya vifaa vya kupimia mionzi. | TZS 200,000/= kwa kazi bila kujumuisha gharama zingine. |
| 2. | Upimaji wa sampuli kwa aidha gamma spectrometry, EDXRF au TXRF | TZS 100,000/ na punguzo la 25% kwa mwanafunzi. |
| 3. | Kwa huduma za kutambua mionzi kwa wafanyakazi | TZS 100,000 kwa kila kitambua mionzi. |
| | Kwa kitambua mionzi kilichopotea | Kitatozwa kwa bei ya soko la kitambua mionzi kwa wakati huo. |
| 4. | Ugezi wa kifaa cha upimaji mionzi, kipimo cha kielectroniki kwa mfanyakazi, kigunduzi cha mionzi kwa mtu binafsi na kwa mazingira. | TZS 150,000/= kwa kila kifaa kwa mkazi bila kujumuisha gharama zingine |
| | | Dola za Kimarekani (USD) 150 kwa kila kifaa kwa asiye mkazi bila kujumuisha gharama zingine |
| 5. | Huduma za ushauri juu ya matumizi sahihi ya mashine za x-rei. | TZS 500,000/= bila kujumuisha gharama zingine. |
| 6. | Ugezi, ukarabati na matengenezo ya vipimo vya unyevu na msongamano na vifaa vingine vya kutoa mionzi | TZS 1,900,000/ kwa kila kifaa bila kujumuisha gharama zingine. |

*Tangazo Na. 478X (Linaendelea)*

| | | |
|---|---|---|
| 7. | Usimikaji, ukarabati na matengenezo ya mashine ya X-rei | TZS 2,500,000/= kwa kila mashine bila kujumuisha gharama zingine. |
| 8. | Kwa usafirishaji, utunzaji na urekebishaji wa mabaki ya vyanzo vya mionzi katika Kituo Kikuu Cha Kuhifadhi Mabaki ya Mionzi (CRWMF) | TZS 4,000,000/= kwa kila chanzo cha mionzi bila kujumuisha gharama zingine. |

Dodoma,
1 Julai, 2022

**ADOLF F. MKENDA**
*Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia*